JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA TANO

02 NOVEMBA, 2026

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA TANO – TAREHE 02 NOVEMBA, 2026

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

60. MHESHIMIWA SHAFFIN AHMEDALI SUMAR (UYUI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya Kata ya Bukumbi, Shitare na Igulungu Jimbo la Uyui.

61. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini tatizo la upungufu wa Walimu katika Shule zetu nchini litakoma.

62. MHESHIMIWA ESTER AMOS BULAYA (BUNDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakarabati Shule za Msingi chakavu zilizopo Jimbo la Bunda Mjini.

63. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa Barabara za Mji wa Karatu kwa kiwango cha lami itaanza kutekelezwa.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

64. MHESHIMIWA ADO SHAIBU ADO (TUNDURU KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya Wahadhiri wa Vyuo Vikuu nchini ili kuboresha ubora wa elimu ya juu.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

65. MHESHIMIWA IBRAHIM MOHAMED SHAYO (MOSHI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupitia upya malipo ya Wapagazi kwani kimekuwa ni kilio cha muda mrefu kwa Vijana.

WIZARA YA NISHATI:

66. MHESHIMIWA ISAYA MOSES MNGURUMI (KONGWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha *line* ya umeme kutoka Zuzu hadi *Substation* ya Mbande Kongwa.

67. MHESHIMIWA ASIA ABDULKARIM HALAMGA (HANANG'):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha kupoza umeme Hanang'.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

68. MHESHIMIWA TUNU JUMA KONDO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali inachukua hatua zipi kutoa elimu kwa mabinti na jamii kuhusu kuripoti vitendo vya udhalilishaji.

WIZARA YA UJENZI:

69. MHESHIMIWA CHARLES JACOB SUNGURA (HANDENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Vibaoni Handeni Mjini - Kang'ata hadi Tuliani yenye urefu wa Km 108.

70. MHESHIMIWA KELLEN ROSE RWAKATARE (MLIMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kivuko cha Kikove – Mlimba.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

71. MHESHIMIWA NASSOR SAID NASSOR (CHAKECHAKE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha Wananchi wanapatiwa vitambulisho vya NIDA bila usumbufu wowote.

72. MHESHIMIWA ASHA OMAR RASHID (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za makazi ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

73. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini dawati maalum la kuwasikiliza na kuwasaidia Vijana wanaokatisha masomo ya Elimu ya Juu kwa kukosa Mikopo litaanzishwa.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

74. MHESHIMIWA SALMA RASHID KIKWETE (MCHINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa Soko la Samaki katika Jimbo la Mchinga.

WIZARA YA MAJI:

75. MHESHIMIWA BARAKA ULIMBOKA MWAMENGO (KYELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Miradi ya Maji ya Ngana *Group* na Mbambo itakamilika.

III. KAMATI YA MIPANGO:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa

unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

(Majadiliano yanaendelea)

DODOMA **BARAKA I. LEONARD**
02 NOVEMBA, 2026 **KATIBU WA BUNGE**